
SUPER GRADE SERIES

MASWALI NA MAJIBU YA MAPAMBAZUKO YA MACHWEO

NA HADITHI NYINGINE



NYAMWEYA O. STEPHEN

kumtembelea ofisini bila Habari.

- **Matusi**. Luka ana fadhila za punda kwa Lilia kwa kumtusi na kumkejeli kuwa ameongeza uzito na kumdhalilisha.

2. <u>Jadili nafasi ya mwanamke kwa kurejelea hadithi ya 'Fadhila za Punda'</u>

<u>i) Nafasi chanya</u>. (Al.10)

- **Mwanamke ni mtetezi wa haki**. Mamake Luka anatetea haki ya Lilia kwa kumsulutisha Luka alete ambulensi haraka.
- **Mwanamke ni msomi**. Lilia anasoma na kuhitimu kuwa mhasibu.
- **Mwanamke ni mwenye bidii**. Lilia anatia bidii masomoni kisha kuhitimu.
- **Mwanamke ni mwenye mapenzi ya dhati**. Mkewe Lee Imani alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe, hali inayomfanya Lee Imai kumkumbuka mkewe kila wakati.
- **Mwanamke ni mwenye msimamo dhabiti**. Lilia anapigania penzi lake kwa Luka bila kukata tamaa.
- **Mwanamke ni mwaminifu**. Lilia ni mwaminifu kwa mumewe Luka kwani hajamwendea kinyume.
- **Mwanamke ni jasiri**. Mamake Luka anadhihirisha ujasiri kwa kumsuta Luka alete ambulensi haraka.
- **Mwanamke ni mwajibikaji**. Mamake Luka anawajibika kwa kumpeleka Luka hospitalini.
- **Mwanamke ni mwenye utu**. Mamake Luka anamwonea Lilia Imani anapopokea kichapo kutoka kwa Luka.
- **Mwanamke ni mlezi mwema**. Mamake Luka anamlea Luka vyema licha ya umaskini.
- **Mwanamke anajali**. Lilia anajali maslahi ya Luka anaposhinikisha Babake hadi kumpa mamake Luka kazi ya kunadhifisha kanisa.
- **Mwanamke ni mvumilivu**. Lilia anavumilia mateso ndani ya ndoa yenye dhuluma. Anapokea kichapo mara kwa mara kutoka ka Luka lakini hakati tamaa.

<u>ii) Nafasi Hasi.</u> (al.10)

- **Mwanamke ni dhaifu**. Mwanamke anaelekezwa na mwanamumme. Lilia anaagizwa asitoke nje na anatii.
- **Mwanamke ni mtawa**. Lilia anatawishwa na Luka, haruhusiwi kutoka nje.
- **Mwanamke nichombo cha starehe.** Luka anarejea kijijini kila mwisho wa wiki kujistarehesha na Lilia.

Nafasi ya mwanamke. Mwanamje anaonyeshwa kuwa mweye utu, mama mkwe
Utu. Mama mkwe anamuuguza Lilia
Ufadhili. Mama mkwe alimfadhili Lilia kwa kumpeleka hospitalini.
Ajira na kazi-Madaktari wanafanya kazi ya kuuguza wagonjwa.

22."Baba, ulimwona kijana yule? Maskini, mavazi hana. Lakini sauti yake sijawahi sikia nyingine kama hiyo."

a. Weka dondoo hili kati kamuktadha wake.(ala.4)

- Ni maneno ya Lilia.
- Kwa Babake Lee Imani.
- Akirejelea Luka
- Lilia anaeleza kuhusu Luka alivyoimba kanisani kwa sauti ya kupendeza na kumvutia Lilia.

b. Fafanua mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (al.4)

- **Swali balagha.** Baba, ulimwona kijanayule?
- **Kinaya**. Luka aliimba kwa sauti mahili kinyume na mwonekano wake.

c. Fafanua umuhimu wa mrejelewa katika hadithi nzima (al.4)

Mrejelewa ni Luka. Fafanua umuhimu wa Luka. Rejelea.

d.Taja na ueleze maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili kwa kurejelea hadithi nzima. (al.12)

Umaskini-Maskini mavazi hana. Fafanua maudhui ya umaskini kwa kurejelea hadithi nzima.

23. "Ili kumridhisha bintiye, ...mhubiri alimwita... Kwanza alimpa tunda ale."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

- Ni maelezo ya mwandishi.
- Kwa msomaji.
- Anarejelea Lee Imani.
- Ni baada ya Lee Imani kumwita Luka nyumbani kutokana na shinikizo la Lilia ambaye alikuwa amevutiwa na Luka.

b. Fafanua sifa mbili za mhubiri zinazojitokeza katika dondoo hili. (al.4)

Mfadhili-anamfadhili Luka kwa tunda.
Mwajibikaji-Anawajibika kumridhisha bintiye kwa kumwita Luka nyumbani.

c. Mbali na ufadhili katika dondoo hili, Fafanua namna wahusika mbalimbali wamefadhiliwa hadithini.(al.12)

- Nafasi za kazi zinatolewa kimapendeleo. Dai anadai kuwa ajira zinawapita zikielekea kwa kina heri wao.
- Ajira husaidia kubadilisha mkondo wa Maisha. Sai anadai kuwa wakipata ajira Maisha yao yatabadilika.
- Kazi hupunguzia watu mawazo. Mzee Makucha anaishabikia kazi yake kwani inampunguzia mawazo na kumsaidia kupitisha wakati.

3.Jadili jinsi haki za binadamu zimekiukwa katika hadithi ya Mapambazuko ya Machweo. (al.20)

- Mzee Makutwa anakiuka haki ya vijana kwa kuwatumikisha migodini wakiwa na umri mdogo.
- Mzee Makutwa anawalipa vijana mshahara duni wanaofanya kazi mgodini. Mshahara ambao vijana hawa wanapata unaishia kuwa lishe.
- Mzee Makutwa anakiuka haki ya vijana kwa kuwafungia mgodini ili wasiweze kutoka. Mgodi huu umezungushwa ua wa stima na kuna majibwa makubwa na walinzi.
- Vijana kwenye mgodi wanalala kwenye mabanda yaliyojengwa kiguu mfano mfano wa zizi la ng'ombe.
- Mzee Makutwa anawajaza vijana kwenye gari bila kuzingatia nafasi kwenye gari hilo.
- Kigogo mhindi anakiuka haki ya Riziki kwa kumwoa katika umri mdogo.
- Mzee Makutwa anakiuka haki ya vijana kwa kuwatumia vibaya vijana wa mtaani na wale wa familia maskini.
- Vijana wenye umri mdogo wanaajiriwa na Mzee Makutwa kuwa dereva. Probox ya Mzee Makutwa inaendeshwa na vijana.
- Mzee Makutwa anakiuka haki ya vijana wanaomfanyia kazi huku wakivalia maguo aliyowazolea njiani.
- Mzee Makutwa anakiuka haki ya elimu anapokatiza masomo ya vijana ili wamfanyie kazi migodini.
- Mzee Makutwa anawatumikisha vijana katika hali ngumu. Vijana wadogo wanajisulubisha pangoni kuchimba madongo na kuyatia kwenye mkokoteni.
- Mzee Makutwa hajali afya ya vijana wanaomfanyia kazi. Mgodini wanafanya kazi katika mazingira yenye joto jingi na uhaba wa hewa.
- Vijana wadogo wanaofanya kazi mgodini wanaamrishwa kwa sauti ya kutisha.
- Vijana wenye umri mdogo wanaajiriwa na Mzee Makutwa kudondoa vijiwe vyenye kung'aa mgodini.
- Vijana mabarobaro wanafanya kazi ya kusukuma matroli yaliyoshiba mchanga kutoka mapangoni.

Rejelea maudhui ya ukiukaji wa haki.

8. "Haya ndugu, endelea kuota jua na kuomba dua."

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

- Haya ni maneno ya Mzee Makutwa
- Anamwambia mwenzake Mzee Makucha
- Wamo barabarani anakochuuza bidhaa mzee Makucha
- Mzee Makutwa anamkejeli mwenzake kuhusu hali yake ya Maisha.

b. Fafanua umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika:

(i)Kujenga Ploti(al.6)

- Anaonyesha Maisha ya awali ya Mzee Makutwa.
- Kupitia kwake inabainika kazi anayoifanya Mzee Makutwa ya kutumikasha vijana.
- Kupitia kwake sifa ya Bi. Macheo inabainika kuwa mshauri mwema.
- Anamjenga mhusika Riziki.

(ii)Kujenga maudhui.(al.10)

- **Uwajibikaji.** Anawajibika kumripoti Mzee Makutwa baada ya kugundua uozo wake.
- **Urafiki.** Alikuwa rafiki mwaminifu wa Mzee Makutwa hapo awali.
- **Bidii.** Anatia bidii katika kutafuta riziki baada ya kufutwa kazi.
- **Ajira na kazi.** Anafanya kazi ya kuuza vitafunio.
- **Madhila ya Maisha.** Anafutwa kazi bila marupurupu.

9."Mlilie binti yako,...si ameolewa na kigogo Mhindi huko ughaibuni?

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)

- Ni maneno ya Mzee Makutwa.
- Kwa Mzee Makucha.
- Ni barabarani anapouzia vitafunio Mzee Makucha.
- Ni baada ya Mzee Makucha kusema hakuna wa kumlilia isipokuwa Mungu ndipo Mzee Makutwa anamwambia maneno haya.

b. Tambua mbinu za uandishi katika dindoo hili.(al.4)

- **Kinaya**- Ni kinaya kwa Riziki kuolewa kwa sababu ya umaskini badala ya kutafuta njia ya kukabiliana nao.
- **Kejeli**-Mzee Makutwa anamkejeli Mzee Makucha eti amlilie bintiye.

c. Fafanua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili.(al.8)

- **Utamaushi**. Bintiye Mzee Makucha anatamauka na kisha kuolewa.
- **Ndoa**. Kigogo mhindi anamwoa Riziki

c. Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (al.8)
Mandhari ni anakoishi Angelica.

- **Uzinzi**. Angelica na Tembo wanazini.
- **Starehe na anasa**- Tembo anafika kwa Angelica Kwenda kujiburudisha.
- **Utapeli**. Angelica anapanga kumtapeli Tembo
- **Tamaa**. Angelica ana tamaa ya mali.
- **Ulaghai**-Angelica anawalaghai wanaumme kwa mwonekano wake.
- **Umaskini**. Mandhari haya yanaonyesha umaskini, chumba ni kibaya.

2. "Maisha yangu hapa hospitalini nitasema yamekuwa mazito kwa upande mmoja na mepesi kwa upande mwingine."

a. Weka dondoo hili katika muktaha wake. (al.4)

- Haya ni maneno ya Tembo
- Akiwa hospitalini
- Anamsimulia Emmi kwenye barua
- Anarejelea hali ngumu ya maisha anayokabiliana nayo.

b. Eleza umuhimu wa mandhari ya hospitalini katika hadithi hii. (al.6)

- **Majuto**. Akiwa hospitalini, Salim anajutia unywaji pombe.
- **Ufadhili**. Salim anamfadhili Tembo kwa kumwandikia barua.
- **Athari za pombe**. Tembo anaathirika kiafya kutokana na unywaji pombe.
- **Ajira na kazi.** Madaktari wanafanya kazi ya kuwahudumia wagonjwa.
- **Mabadiliko**-Hali ya Tembo inabadilika na anaendelea kupata nafuu.

c. Tibitisha ukweli kuwa Maisha hospitalini ni mepesi na wakati huo magumu.

(i)Maisha kuwa mepesi.

- Afya ya Tembo inaimarika.
- Tembo ana rafiki anayemwandikia barua, Salim.
- Tembo anatembelewa akiwa hospitalini.
- Amefanya marafiki humo kwa mfano muuguzi Nasir
- Nasir anamhudumia na ana moyo mkubwa
- Anampata Salim ambaye anamhimiza na kumtia matumaini
- Anampata Salim ambaye anamsaidia kuandika waraka kwamkewe Emmi
- Anatibiwa na kupata nafuu
- Bado yu hai ilahali wenzake walishaaga.

- **Ukosefu wa muda wa kutosha**. Sabina anakosa muda kwa kutosha kusoma kutokana na kazi nyingi nyumbani.
- **Kukataliwa baada ya kupewa mimba**. Mwanamume aliyempa Nyaboke ujauzito anamkaa.

2.'Jamii imemkandamiza mtoto wa kike' Fafanua kwa mujibu wa hadithi ya Sabina.(al.20)

Kupigwa. Yunuke anamdhulumu Sabina Manoti kwa kumpiga. Anampiga sana baada ya kutoka shuleni bila kosa.
Kutaka kuozwa. Ombati anamdhulumu Sabina kwa kutaka aolewe mapema ilia pate mahari.
Kazi nyingi. Yunuke anamkandamiza Sabina kwa kumpa kazi nyingi za nyumbani.
Kutojali. Yunuke hajali iwapo Sabina anapata muda wa kutosha wa kudurusu.
Kazi za kuchosha. Kazi anazofanya Sabina ni za kuchosha katika umri wake.
Dhuluma za kimapenzi. Nyaboke anadhulimiwa kimapenzi na mwanamme anayempa ujauzito kisha kumtoroka.
Kuzomewa. Yunuke anamdhulumu Sabina kwa kumzomea na kumtukana kutokana na kufika nyumbani akiwa amechelewa
Kunyimwa nafasi ya kusoma. Sabina hapati nafasi ya kutosha ya kudurusu kutokana na kazi nyingi.
Kukimbiwa. Mwanamume anayemtunga mimba Nyaboke anamdhulumu kwa kumtoroka.
Kukosa muda wa kubarizi. Yunuke anamdhulumu Sabina kwa kutompa muda wa kubarizi hata kidogo kwa kulimbikiziwa kazi nyingi.
Fujo. Sabina anapoketi chini ya mparachichi kupumzika, Yunuke anamdhulumu kwa kumwita kwa fujo.
Kutosaidiwa. Hata binamu zake Sabina wanamdhulumu kwa kutomsaidia wanapokuja likizo.
Kuvamiwa. Sabina anapochelewa kwa mwalimu mkuu, Yunuke anamdhulumu kwa kumvamia japo anamwambia ni barua imemchelewesha.

3.Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wamewajibika katika hadithi ya Sabina.

- Mwalimu mkuu anawajibika kuwapa wanafunzi ushauri kwamba hawafai kufika shuleni wakiwa wamechelewa wakati wa mtihani.
- Wanafunzi wanawajibika kwa kufika shuleni mapema ili kuanza mtihani wao wa kitaifa wa darasa la nane.

11. Fafanua matumizi ya kisengerenyuma katika hadithi ya kifo cha Suluhu.

- Abigael anakumbuka kuwa amewahi kuwa chumbani waliko awali.
- Abigael anakumbuka kauli za Suluhu kuhusu saa yake aliyodai alinunua dola elfu kumi.
- Abigael anapochukua dawa ya kumtilia kwenye kinywaji, anakumbuka maagizo ya Natasha.
- Suluhu na Abigael walikuwa wamekaa katika uhusiano wao kwa mwaka na kila kijusi kilipotunga walikiondoa.
- Abigael anapotoa kisu kwenye mfuko wake, anakumbuka ulinunuliwa mfuko huo na Suluhu kama ishara ya penzi lao.
- Abigae katika chumba cha kuzini Anakumbuka agizo la kuurudisha mkoba wake kwa Suluhu mapenzi hayo yakifa
- Bi. Suluhu anamkumbusha mumewe kule walikotoka.
- Bi Suluhu Anakumbuka Suluhu akiuza makaa ndoa yao ilipoanza,
- Bi. Suluhu Anakumbuka jinsi na biashara ya kuuza makaa ilivyosambaratika baada ya ukataji miti kupigwa marufuku.
- Suluhu anamkumbusha binti wa chuo kikuu aliyemtia mimba na kumtelekeza na hawara aliyempangia chumba mjini.
- Suluhu anamkumbusha kuwa alimuua mamake Abigael baada ya kunyakua shamba lake.
- Suluhu Anakumbuka kuwa Bwana Ngoma alimkopesha pesa za kampeni .
- Suluhu Anakumbuka kuwa aliwasahau raia baada ya kumpigia kura.
- Suluhu Anakumbuka msaada aliowapa Wazazi wa mkewe kabla ya ndoa yao.

12. Fafanua umuhimu wa wahusika wafuatao katika hadithi ya 'Kifo Cha Suluhu'

(i)Abigael. ***Anaonyesha*:**

- **Uzinzi**-ana uhusiano wa kimapenzi na Suluhu.
- **Changamoto wanazopitia wanafunzi-** kama vile umaskini.
- **Ukatili**-Abigael ananuia kumuua Suluhu ili ampore pesa.
- **Utegemezi**-Abigael anawategemea wanaume ili kupata pesa.

(ii) Bi Suluhu. ***Anaonyesha***:

- **Changamoto za ndoa**. Bi.Suluhu katika barua anadokeza namna mumewe amejitenga naye.
- **Uwajibikaji**. Serikali inapiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la dafrau.
- **Malezi.** Suluhu anawalea wanawe pekee hadi wakamaliza shule.